


Latra: Nauli ya Sh 1,000/- mwendokasi ni ya mpito



Na Mwandishi Wetu

MKURUGENZI Mkuu wa Mam-laka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo (pichani) amesema nauli ya Sh 1,000 inayotumika katika mabasi yaendayo haraka ni ya mpito.

Suluo alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha, akitoa ufafanuzi

kuhusu kiwango hicho cha nauli.

Alisema nauli hiyo inayotumika sasa iliridhiwa kuwa Sh 1,000 kwa tangazo la Serikali la Agosti 29, mwaka huu.

Alifafanua kuwa nauli hiyo ni ya mpito wakati Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ukiendelea kukusanya mapendekezo kutoka kwa wadau ili kuja na nauli ya kudumu.

"Nauli hizi ni za mpito mpaka pale ambapo Dart atakapowasilisha maoni. Tutaita wadau ili kuona mapendekezo ya Dart baada ya kukaa na watoa huduma kuhusu kiwango sahihi cha nauli. Tunaposema ya mpito, nauli hii inamtosheleza mtoa huduma asipate hasara wala faida," alisema.

Suluo alisema kiwango hicho cha nauli ya mpito kimewekwa ili kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania, akisema kinyume chake itakuwa vigumu watu kuja kufanya biashara nchini kutokana na mazingira kutolipa.

Alisema kiwango hicho cha nauli hakihusiani na matukio ya Oktoba 29, mwaka huu, bali matukio ya siku hiyo yalisababisha uharibifu wa miundombinu wakati tangazo la nauli

lilikuwa limetolewa tangu Agosti.

"Ni kwamba imezoeleka Latra ndiyo hutangaza, lakini Dart walitangaza na sisi tukaridhia, na tangazo likachapishwa kwenye Gazeti la Serikali," alifafanua.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Dart, Said Tunda alisema nauli ya Sh 1,000 ndiyo kiwango kinachoweza kumvutia mwekezaji kuleta mabasi, akieleza kuwa jukumu la serikali ni kujenga miundombinu, huku mabasi yakiendeshwa na sekta binafsi.

"Tupo kwenye mstari, kwa sababu nia si kuwau-miza wananchi. Baada ya huduma kusimama, watu walikuwa wakilipa kati ya Sh 5,000 hadi Sh 6,000 kwa safari ambayo sasa in-alipiwa Sh 1,000," alisema.

Rapid transit 1,000/- fare temporary, says regulator

FROM PAGE 1

that high passenger volumes will sustain operations and attract more investors into the sector.”

The primary objective of setting the transitional fare was to restore public confidence in the BRT system and encourage wider private sector participation in its operations, he said, commending DART for addressing operational challenges delaying service delivery.

This was particularly the case for Phase Two of the BRT project, with improvements in fare collection system and availability of buses significantly enhancing service reliability, he stated.

He said that LATRA conducted an inspection of BRT Phase Two and witnessed operational challenges which have since been resolved thus enabling restart of services, noting that DART conducted those improvements and strengthened the fare collection system.

This had increased the number of buses as 60 buses are now redeployed on BRT Phase One routes, he said, while Said Tunda, the DART chief executive officer, said that the government had prioritised citizens' welfare by keeping fares affordable despite infrastructure setbacks that disrupted services.

This interim fare is reasonable as the goal is not to burden commuters but to ensure the provision of reliable and sustainable public transport, he said, underlining that before the resumption of BRT services, passengers were paying as much as 6,000/- on a long range trip by seeking out motorcycles or tricycle modes of transport.

Under LATRA regulations on charges issued in 2020, transport service providers are required to publicly announce any new fares at least 14 days before implementation through mass media channels accessible to the public, he added.

Utukue Jumat Desemba 19, 2025 Pg 2

neo mbalimbali

'Buku' nauli ya mpito mwendokasi-LATRA

Dar es Salaam
NA MWADISHI WETU

MKURUGENZI Mkuu Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Dk. Habibu Suluo, amesema sh. 1,000 wanazotozwa abiria wanaotumia usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT), ni nauli ya mpito.

Dk. Suluo alisema nauli halisi zitatumika baada ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), kuwasilisha maombi ya nauli mpya.

Dk. Suluo alisema hayo katika Maonesho ya Mkutano wa 18 wa Tathmini ya Utendaji Kazi wa Sekta ya Uchukuzi, uliofanyika Ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), jana.

"Nauli ya mpito ya BRT iliridhiwa sh. 1,000 kwa Tangazo la Serikali la Agosti 29, 2025 na hii ilikuwa inawapa uhakika wale wanaoleta mabasi kwamba nauli hii (1,000) wanaweza wakaanza nayo hadi pale DART itakapoleta maombi rasmi ya mapendekezo ya nauli



Mamlaka ilifanya ziara ya mradi wa BRT awamu ya pili na kabla ya kutangazwa nauli ya sh. 1,000, kulikuwa na changamoto kwenye uendeshaji ambapo changamoto hiyo ilitatuliwa na huduma za usafiri zikaanza kutolewa.

Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Dk. Habibu Suluo

baada ya kukaa na watoa huduma ya usafiri huo.

Kwa sasa nauli hizi zinamtosheleza mtoa huduma kutopata hasara, lakini kutopata faida ili aingie sokoni. Anaweza akaona faida kwa sababu abiria ni wengi, lengo la kuweka nauli hii ni kuwavutia wawekezaji wengine kutoa huduma," alisema Dk. Suluo.

Aliipongeza DART kutatua changamoto zilizobainika awali na kufanikisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

"Mamlaka ilifanya ziara ya mradi wa BRT awamu ya pili na kabla ya kutangazwa nauli ya sh. 1,000, kulikuwa na changamoto kwenye uendeshaji ambapo changamoto hiyo ilitatuliwa na huduma za usafiri zikaanza kutolewa.

Tunawapongeza na kuwashukuru kwa uboreshaji wa BRT awamu ya pili katika mfumo wa kukusanya nauli pamoja na mabasi kuwa mengi, hali iliyosababisha mabasi 60 kuazimwa kwenda BRT awamu ya kwanza," alisema.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu DART, Said Tunda, alisema serikali inawajali wananchi, ndiyo maana baada ya kuharibika miundombinu iliyosababisha changamoto ya usafiri kwa wananchi, huduma zinaendelea katika vituo vingi vya mwendokasi kwa kulipia gharama sh. 1,000.

Mtendaji huyo alisema nauli sh. 1,000 inafaa kwa kuanzia kwa sababu lengo si kuwaumiza watumia huduma, ni kuhakikisha abiria wanapata huduma bora na endelevu.